

**HOTUBA YA MHE. OMAR SAID SHAABAN (MBW), WAZIRI WA BIASHARA
NA MAENDELEO YA VIWANDA, SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
KATIKA WA SHEREHE ZA KUFUNGA MAONESHU YA 46 YA KIMATAIFA
YA BIASHARA YA DAR ES SALAAM TAREHE 13 JULAI, 2022 KATIKA
UWANJA WA MWL. J.K. NYERERE, DAR ES SALAAM**

***Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya
Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda
na Biashara;***

Waheshimiwa Mawaziri wote mliopo hapa;

***Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe (Mb.), Naibu Waziri wa Uwekezaji,
Viwanda na Biashara;***

Waheshimiwa Manaibu Waziri wote mliopo hapa;

Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Mheshimiwa Jokate Mwegelo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke;

***Prof. Godius Kayharara, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na
Biashara;***

Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wote Mliopo hapa;

Waheshimiwa Mabalizi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa;

Prof. Ulingeta Mbamba Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TanTrade;

Bi. Latifa Khamis, Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade;

***Bi. Angelina Ngalula Mwenyekiti na Mwakilishi wa Sekta Binafsi Tanza-
nia;***

***Bi. Esther Mang'anya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania na wad-
hamini wakuu wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es
Salaam;***

Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini Mlioko hapa;

Viongozi wa Mashirika ya Umma na Binafsi;

Menejimenti ya Wizara na TanTrade;

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi TanTrade

Ndugu Washiriki wa Maonesho;

Wageni Waalikwa;

Wanahabari;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Nami niendeleo kuungana na wenzangu waliotangulia, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kujumuika katika siku hii ya leo.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika hafla ya kufunga Maonesho haya.

Nimshukuru Waziri mwenzangu, **Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara** na Menejimenti ya TanTrade chini ya **Bi. Latifa Mohamed Khamis** Mkurugenzi Mkuu, kwa kunialika tena kuja kujumuika nanyi leo kwenye ufungaji wa Maonesho haya makubwa. Nilikuja kipindi cha ufunguzi wa Maonesho tarehe 03 Julai, 2022 na leo nipo tena, hakika nimefarajika kuwepo hapa na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Nimepewa nafasi hii kwa lengo la kukushukuru wewe Mheshimiwa Mgeni Rasmi lakini pia kuleta salamu kutoka Zanzibar. Na kwa vile pia

Wizara yangu inashughulikia masuala ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, niseme nimefurahishwa sana na uwepo wa Maonesho haya ambayo kwa hakika yametoa fursa kwa Watanzania kujitangaza, kujifunza, kupata teknolojia mpya lakini zaidi kujenga mitandao ya kibiashara na Washiriki mbalimbali kutoka ndani na nje ya Nchi.

Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na Banda maalumu lililoratibiwa chini ya Wizara yangu lililokuwa na Washiriki kutoka Zanzibar. Ni imani yangu kuwa washiriki wetu hawajatoka bure, wamepata vingi kutokana na ushiriki wao katika Maonesho haya.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Nikuahidi wewe na Serikali kwa ujumla, kuwa tutaendelea kudumisha ushirikiano baina ya Wizara zetu hizi mbili katika kuhakikisha tunakuza Sekta hii ya Biashara na Viwanda kwa maslahi mapana ya Wananchi waliotupa dhamana ya kuwaongoza, na Taifa letu kwa ujumla. Na kwa hili naomba nikudokeze, tunao Mpango wa kujenga Uwanja wa Maonesho wa Kisasa na wa kimataifa katika eneo la Fumba Zanzibar, ambao utatoa fursa kwa bidhaa zetu kuendelea kutangazwa na kujulikana na mataifa mbalimbali. Zanzibar pia kuna fursa mbalimbali za kibiashara na uwekezaji zikiwemo za Kilimo, Utalii na Uchumi wa Buluu ambayo kwa sasa ndio Sera kuu ya **Mhe. Dkt. Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar**. Tutashirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo TanTrade katika kuendeleza Uwanja huo na pia katika uratibu wa Maonesho mbalimbali ili kufikia malengo

tuliyojiwekea kwa kasi zaidi maana wao wameshakuwa wazoefu katika Sekta hii.

Basi baada ya kusema hayo Mheshimiwa Mgeni Rasmi, nishukuru tena kwa kuwepo kwako mahali hapa, na niwakaribishe wote Zanzibar.

**Asanteni kwa kunisikiliza!
Kazi Iendele...!**